



JE! WAJUA? UFUGAJI WA VIPEPEO KIBISHARA HUCHOCHA MAENDELEO YA JAMII NA UHIFADHI WA MAZINGIRA

Wafugaji wa Vipepeo Amani Tanga, wanaweza kupata hadi Sh. 90,000,000 kwa mwaka! Kwa wastani biashara ya vipepeo husaidia kila mfugaji kuongeza kipato cha kati ya Shilingi 80,000 mpaka 200,000 kwa mwezi.



Hatua za ukuaji wa vipepeo

Baada ya buu kupasuka, kipepeo hutokea akiwa kwenye hali ya ubichi kwenye mbawa zake. Baada ya kukauka kwa bawa, kipepeo huonekana mkubwa na mkakamavu na kuanza kuruka kwenye maua kujitafutia chakula na kujamiiana, Katika hatua hii, mfugaji wa vipepeo anaweza kujipatia fedha kwa njia maonesho

Katika ufugaji wa vipepeo kibishara, kwa kawaida huuzwa wakiwa katika hatua ya ukuaji inayoitwa Buu. Buu huuzwa katika masoko ya ulaya na kuingiza fedha za kigeni, ambazo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi.

UTAWEZAJE KUFUGA VIPEPEO?

Katika kuandaa shamba la ufugaji wa vipepeo kibiashara, zingatia hatua zifuatazo:

HATUA YA 1:

Maandalizi ya eneo la kufugia vipepeo.

- Andaa banda au shamba lenye mzunguko wa kipenyo cha mita 12 hadi 13
- Panda maua ya mimea ndani ya shamba au banda la kufugia vipepeo ambayo hutumiwa na vipepeo kujipatia chakula na kutagia mayai
- Zungushia shamba au banda la kufugia vipepeo kwa kutumia uzio wa mimea yenye maua
- Weka mazingira mazuri hasa maua na majani yanayovutia vipepeo jike kutua na kuweza kutaga mayai
- Weka mazingira mazuri kwa viwavi kujipatia chakula. Mazingira hayo yawe na maji maji, mimea, majani ya miti na maua



HATUA YA 2:

Chagua aina ya vipepeo unaopendelea kuwafuga

Unaweza kuchagua vipepeo wanaweza kuishi muda mrefu, muda mfupi au vipepeo ambao mayai yao huchukua muda mfupi kubadilika kuwa kiwavi, buu na hatimae kipepeo

HATUA YA 3:

Hakikisha mabuu hayaathiriwa na wadudu

Unaweza kuhamisha mabuu kutoka sehemu isiyo kuwa salama kwenda sehemu yenye usalama zaidi ndani ya banda au shamba, sehemu ambayo haina wadudu kama mchwa na sisimizi, kuwaweka kwenye kichanja kilichopo ndani ya banda na kuwapatia maji.

HATUA YA 4:

Nyunyizia maji kidogo kwenye mabuu

Nyunyizia mabuu angalau mara mbili (2) hadi tatu (3) kwa wiki hadi pale litakapo badilika kuwa kipepeo. Mabuu hunyunyiziwa maji ili yasikauke sana

HATUA YA 5:

Kusanya mabuu tayari kwa kuuzwa

Kwenye hatua hii, mfugaji wa vipepeo atakusanya mabuu yote, atayachambua na kuyaweka kwenye vifungashio kwa ajili ya kusafirishwa kwa ajili ya biashara



Imeandaliwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa Ufadhili wa Mradi wa Kuongeza Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu Tanzania
Kwa Mawasiliano zaidi: Mkurugenzi Mtendaji; Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA); S.L.P 21522 Dar-es-Salaam – Tanzania; tovuti: www.mjumita.org barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org



Kwa ufadhili wa ushirikiano wa Tanzania na Finland